# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA

Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz

Website www.humanrights.or.tz


**Machi 1, 2018**

## TAARIFA YA UANGALIZI WA UCHAGUZI MDOGO WA MARUDIO KWA MAJIMBO YA KINONDONI NA SIHA

Katika kufikia maono ya kupata jamii yenye haki na usawa, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeendelea kufanya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa serikali katika kipindi cha uchaguzi mdogo katika majimbo ya Siha na Kinondoni. Mnamo Februari 9, 2018 Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilipata kibali rasmi kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa mwangalizi wa uchaguzi katika jimbo la Kinondoni pamoja na Siha.

Katika kutimiza jukumu hilo la kidemokrasia, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimefanya uangalizi tangu zilipoanza kampeni mnamo tarehe 25/01/2018 na wakati wa uchaguzi ambapo katika chaguzi hizo ndogo Chama cha Mapinduzi kilishinda. Hata hivyo Kituo Cha Sheria na Haki za Binadamu kimebaini masuala kadhaa ya ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa sheria na taratibu zinazoratibu chaguzi kama yalivyofafanuliwa:-

<u>Kipindi cha Kampeni za Uchaguzi:</u>

1. **Matumizi ya watoto katika kampeni**

Kwa mujibu wa kifungu namba 12 cha Sheria ya Mtoto, 2009 kinakataza kuwaajiri au kumtumia mtoto katika shughuli yoyote ile ambayo ni hatarishi kwa maslahi mapana ya mtoto, kiafya, kielimu kiakili, kimwili pamoja na maendeleo ya kimaadili. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshuhudia video ya mtoto mdogo aliyekuwa jukwaani akitumika kutumbuiza katika mkutano wa kampeni wa Chama cha Mapinduzi (CCM) uliofanyika Makumbusho katika jimbo la Kinondoni Februari 2, 2018. Huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu hususani haki za watoto.

2. **Matumizi ya rasilimali za Umma kwa maslahi ya vyama**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kupitia waangalizi wa Uchaguzi kimeshuhudia viongozi wa serikali wakitumia magari ya umma katika mikutano ya kisiasa kinyume na Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria za Uchaguzi haswa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010. Katika Jimbo la Siha mnamo Februari 16, 2018, eneo la Sanya juu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilishuhudia magari ya Umma yakitumika katika kumnadi mgombea ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ndugu Alloyce Mollel ambapo Waziri wa Ardhi

Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mh. William Lukuvi aliambatana na msafara wenye magari ya Umma.

**2. Matumizi ya nguvu yaliyopelekea watu kujeruhiwa na kuuawa**

Matumizi ya nguvu zaidi yameshuhudiwa katika kipindi cha kampeni na kupelekea raia kuumizwa na hatimaye vifo. Katika jimbo la Kinondoni mnamo Februari 16, 2018 eneo la Mkwajuni mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji (NIT) aliyefahamika kwa jina la Akwilina Baftah aliuawa kwa kupigwa risasi kufuatia polisi kutumia risasi kuwasambaratisha waandamanaji wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) waliondamana kudai viapo vya uwakala katika jimbo la Kinondoni. Sambamba na hilo jeshi la Polisi liliendelea kuwashikilia wafuasi 40 wa CHADEMA wakiwemo wanawake wenye watoto wadogo na majeruhi wawili (2) wa risasi. Kwa upande wa Jimbo la Siha Polisi walimpiga mwanamke mmoja aliyefahamika kwa jina la Husna Said na kupelekea kuvunjika mguu.

<u>Kipindi cha Uchaguzi:</u>

Katika uangalizi wa siku ya uchaguzi Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kupitia kwa waangalizi wake kiliweza kubaini masuala yafuatayo:-

**1. Mwitikio mdogo wa wapiga kura**

Katika zoezi zima la uangalizi waangalizi wameweza kuona idadi kubwa ya watu wakijitokeza zaidi katika kampeni za vyama vya siasa na sio siku ya kupiga kura. Kwa upande wa jimbo la Kinondoni katika idadi ya waliojiandikisha 264,055, ni watu 45,454 waliojitokeza kupiga kura sawa na asilimia 17 na kwa Upande wa jimbo la Siha watu waliojiandikisha ni 55,313 na waliojitokeza kupiga kura ni 32,277 sawa na asilimia 58. Hii inafanya idadi ya jumla ya wapiga kura katika majimbo yote kuwa asilimia 24 pekee ya waliojiandikisha.

**2. Unyanyasaji wa mawakala wa vyama vya siasa**

Siku ya uchaguzi tarehe 17/02/2018 Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kupitia waangalizi wake kilishuhudia baadhi ya mawakala kunyanyaswa kwa kunyimwa kuingia katika chumba cha kupigia kura pasipo sababu za msingi ikiwemo barua zao za viapo kukosa sahihi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi. Jimbo la Siha hali hii ilishuhudiwa katika Kituo cha Nasai Shule ya msingi ambapo mawakala wa, CUF na SAU na CHADEMA walizuiliwa kuingia katika chumba cha kupigia kura bila kupewa sababu za msingi. Februari 16, 2018 katika Jimbo la Kinondoni pia Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilishuhudia katika baadhi ya vituo mawakala wa vyama kutokupewa kwa wakati viapo kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni na kusababisha usumbufu wakati wa zoezi la uchaguzi.

3. **Uwezo wa Wasimamizi wa Uchaguzi**

Katika zoezi la uongozaji wapiga kura katika vituo kumekuwa na changamoto za kiutendaji miongoni mwa wasimamizi wa uchaguzi chini ya Tume ya Uchaguzi. Tumeshuhudia baadhi ya Wasimamizi wa Uchaguzi kuwazuia na kuwakataza watazamaji wa ndani wa uchaguzi kuingia katika chumba cha kupigia kura kinyume na Kifungu namba **63(1) (f)** cha Sheria ya Uchaguzi sura namba 343 ambacho kimetaja mwangalizi

pamoja na watu wengine wanaoruhusiwa kuwepo katika chumba cha kupigia kura. Hii imeshuhudiwa katika vituo vya Kibongoto, Levishi pamoja na Nasai vyote katika Jimbo la Siha ambapo wasimamizi wa uchaguzi katika vituo hivyo hawakutoa ushirikiano kwa waangalizi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa kutokujua sheria au kwa makusudi.

**4. Mazingira yasiyo rafiki kwa wapiga kura na watu wenye ulemavu.**

Katika baadhi ya vituo ambavyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilifanya uangalizi tulibaini vituo kutokuwa na mazingira wezeshi kwa wapiga kura. Vituo hivyo kutokuwa na mazingira wezeshi kunadidimiza haki za makundi maalumu ikiwemo watu wenye ulemavu wa viungo, wazee na wanawake wenye ujauzito. Mazingira duni ya vituo vya kupiga kura pia yanapelekea kukiukwa kwa taratibu za kupiga kura ikiwemo kukosekana kwa usiri wakati wa kupiga kura. Katika Jimbo la Siha kituo cha Levishi hakikuwa na nyenzo rafiki na wezeshi kwa watu wenye ulemavu kuweza kufika na kupiga kura, pia katika eneo la Karansi kituo cha Usharika ambapo chumba cha kupigia kura hakikuwa na mwanga wa kutosha na usiri wa mpiga kura na hivyo mawakala walionekana wakiwaelekeza wapiga kura katika chumba cha kupigia kura.

5. **Uwepo wa Mabango katika vituo vya kupigia kura.**

Sheria ya Uchaguzi sura namba 343 inakataza uwepo wa mabango au bendera za vyama vya siasa katika kituo cha kupigia kura. Hali hii imeonekana na waangalizi wetu katika Jimbo la Siha kituo cha kupigia kura cha Lawate ambapo bendera za vyama vya siasa ikiwemo Chama cha Mapinduzi na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

6. **Kutokuwepo na usiri katika eneo la kupigia kura**

Zoezi la kupiga kura linaitaji usiri kwa mpiga kura ili kuwezesha uchaguzi huru na wenye Haki. Waangalizi wameshuhudia ukiukwaji wa haki hii ya msingi katika uchaguzi huu mdogo. Jimbo la Siha katika eneo la Karansi kituo namba 2 cha kupigia kura kilichopo Chama cha Ushirika chumba kilikuwa kidogo na mwanga hafifu na pia kutokana na udogo kutokuwepo na usiri hali iliyopelekea mawakala wa vyama kuanza kuwaelekeza wapiga kura kiuwazi zaidi. Hali hii pia ilijitokeza katika jimbo la kinondoni ambapo kituo cha kupigia kura kiliwekwa katika kituo cha mabasi ya mwendokasi.

7. **Uwepo wa Polisi wengi Vituoni**

Katika zoezi zima la upigaji kura waangalizi wetu wameshuhudia uwepo wa askari wengi wenye silaha za moto katika baadhi ya vituo vya kupigia kura. Kwa upande wa Jimbo la Siha eneo la Ngarenairobi na Nasai kulishuhudiwa polisi wengi wakiwa vituoni jambo ambalo linaweza kuwa sababisha hofu kwa wapiga kura hasa kwa kuzingatia tukio la maujai lililojitokeza kabla ya uchaguzi.

**7. Kupotea kwa Sanduku**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kupitia waangalizi wake waliokuwepo katika eneo la Kituo cha Idrisa walishuhudia tukio la sanduku la kupigia kura kuibwa au kuondolewa na baadaye kurejeshwa na zoezi la upigaji kura kuendelea na sanduku hilo hilo likaendelea kutumika. Tukio hili limetia dosari uchaguzi kuwa wa huru na haki miongoni mwa wapiga kura na wananchi kwa ujumla.

8. **Vituo kutokufunguliwa kwa wakati.**

Sheria ya Uchaguzi sura namba 343 imetamka muda wa zoezi la upigaji kura kuanza saa 1 kamili asubuhi mpaka saa 10 kamili jioni, lakini katika zoezi la uangalizi kwa Upande wa Jimbo la Siha Kituo cha Levishi Hospitali zoezi lilichelewa kuanza ambapo kituo kilifunguliwa mnamo saa 2 asubuhi jambo ambalo linaweza kupelekea baadhi ya wananchi kukosa haki yao kwa sababu za muda kutokutosha.

Hivyo kwa changamoto hizo mbalimbali zilizotijokeza Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaona kuwa uchaguzi ulikuwa huru lakini sio wa haki.

**Mapendekezo:**

Kwa kutambua uwepo wa changamoto zilizoainishwa hapo juu, Kituo cha Sheria na Haki za kinatoa mapendekezo yafuatayo ili kuwepo kwa uchaguzi huru na wa haki:-

1. Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuratibu chaguzi mbalimbali kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zilizopo bila kufungamana na itikadi zozote za vyama vya siasa;
2. Tume ya taifa ya uchaguzi kutumia maafisa wake waliopata mafunzo stahiki katika zoezi zima la usimamizi na sio kutumia watu wasio na uelewa wa sheria za uchaguzi na kanuni zake;
3. Tume ya taifa ya uchaguzi kutoa elimu ya mpiga kura ili kuwezesha wananchi kufahamu sheria na taratibu za uchaguzi;
4. Vyama vya siasa hasa chama tawala kuacha matumizi ya rasilimali za umma hasa katika kipindi cha kampeni;
5. Vyama vya siasa kujikita katika kuhubiri ilani za vyama vyao na kuacha kutumia kejeli matusi pamoja na vijembe katika kuomba kura kwa Wananchi;
6. Vyama vya siasa kuacha kulinda na kuheshimu sheria za uchaguzi na sharia nyingine za nchi ikiwemo kujiepusha na matumizi ya watoto katika majukwaa ya kisiasa;
7. Jeshi la polisi kuacha matumizi ya nguvu yaliyopitiliza na silaha za moto katika kutimiza majukumu yao ili kulinda haki za msingi ikiwemo haki ya kuishi;
8. Jeshi la polisi kuwa huru na kutokufungamana na siasa za vyama au kupokea maagizo yasiyohalali yanayolinda maslahi ya chama/kundi fulani;
9. Jeshi la polisi kuwa walinzi wa Amani na usalama wa raia na sio kuwa wachochezi wa vurugu na kuumiza raia;
10. Masajili wa vyama kutimiza majukumu yake ya kuviwajibisha vyama vinavyokiuka sheria na taratibu wakati wa kampeni;
11. Wananchi kuheshimu sheria, taratibu na kanuni mbalimbali zilizowekwa ili kudumisha amani na utulivu hasa kipindi cha uchaguzi

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua madhaifu yaliyopo katika sheria zetu za uchaguzi na tunapendekeza kufanyika kwa maboresho ya sheria na taraibu hizo ili kuboresha chaguzi zijazo ikiwemo wa 2019 na 2020.

**Imetolewa na;**

**Anna Henga**
**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**